
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# SERA YA TAIFA YA MENEJIMENTI YA MAAFA



OFISI YA WAZIRI MKUU
S.L.P 3021 DAR ES SALAAM
SIMU: 022 2117249-53
FAX: 022 2117266
E-mail: ps@pmo.go.tz

# Mafuriko


30
35
40
-5
-10
Lake Victoria
MARA
KAGERA
MWANZA
SHINYANGA
KIGOMA
TABORA
SINGIDA
DODOMA
MANYARA
KILIMANJARO
TANGA
PEMBA
ZANZIBAR
DAR ES SALAAM
Indian Ocean
MOROGORO
RUKWA
Lake Rukwa
MBEYA
RUVUMA
LINDI
MTWARA
Lake Nyasa
Kaskazini
Skeli 1:5,000,000
Kielelezo
Kidogo sana
Kidogo
Kubwa
Kubwa sana
Maeneo ya Maji
Mpaka wa Mkoa
Mpaka wa Wilaya

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# SERA YA TAIFA YA MENEJIMENTI YA MAAFA

OFISI YA WAZIRI MKUU
S.L.P 3021 DAR ES SALAAM
Simu: 022 2117249-53
Fax: 022 2117266
E-mail: ps@pmo.go.tz

# YALIYOMO


1.0 Sura ya Kwanza: Utangulizi ........................................ 1

1.1 Umuhimu wa sera ........................................ 1

1.2 Madhumuni na Upeo wa Sera ........................................ 2

2.0 Sura ya Pili: Matamshi ya Sera ........................................ 3

**2.1 Vipengele vya menejimenti ya maafa ........................................ 3**

2.1.1 Kuzuia na kupunguza athari ........................................ 3

2.1.2 Kujiandaa kukabiliana na Maafa ........................................ 4

2.1.3 Kukabili Maafa ........................................ 5

2.1.4 Kurejesha Hali ........................................ 6

2.1.5 Tathmini Baada ya Maafa Kutokea ........................................ 7

2.1.6 Upatikanaji wa Fedha ........................................ 7

2.1.7 Mambo ya Ujumla ya Kisera ........................................ 8

2.1.7.1 Makundi Maalum ........................................ 8

2.1.7.2 Ushirikiano wa Kikanda ........................................ 9

2.1.7.3 Mifumo ya Tahadhari ........................................ 10

2.1.7.4 Misaada kwa Waathirika wa Maafa ........................................ 11

2.1.7.5 Hifadhi ya Mazingira ........................................ 12

3.0 Sura ya Tatu: Muundo wa Menejimenti ya Maafa ........................................ 13

**3.1 Maelezo ya Jumla ........................................ 13**

3.1.1 Kamati za maafa ........................................ 13

3.1.2 Tume ya Menejimenti ya Maafa ........................................ 13

3.1.3 Asasi Ongozi ........................................ 14

3.1.4 Kamati za Kitaalam ........................................ 14

3.1.5 Vitengo vya Menejimenti ya Maafa ........................................ 14

3.1.6 Timu za Kukabili Maafa ........................................ 14

3.1.7 Ngazi ya Jamii ........................................ 14

**3.2 Wajibu na Majukumu ya Wadau Wengine: ........................................ 14**

3.2.1 Vikosi vya Ulinzi na Usalama ........................................ 15

3.2.2 Ushiriki wa Sekta Binafsi ........................................ 15

3.2.3 Idara ya Zimamoto na Uokoaji ........................................ 15

3.2.4 Jeshi la Polisi ........................................ 15

3.2.5 Asasi zisizo za Kiserikali ........................................ 16

3.2.6 Taasisi za Kimataifa ........................................ 16

3.2.7 Vyombo vya Habari .................................... 16
3.2.8 Ngazi ya Jamii na Familia .................................... 17
3.3 Taratibu za Kisheria .................................... 17
3.4 Ufuatiliaji na Tathmini .................................... 17
3.5 Majumuisho .................................... 18

Kiambatisho Na. 1 Muundo wa Menejimenti ya Maafa .................... 19
Kiambatisho Na. 2 Majukumu ya Kamati na Wadau Wengine ...... 20

1.0 Tume ya Menejimenti ya Maafa .................................... 20
1.1 Jukumu la Jumla .................................... 20
1.2 Majukumu Mahususi .................................... 20

2.0 Muundo katika Mikoa na Majukumu .................................... 21
2.1 Kamati ya Menejimenti ya Maafa ya Mkoa .................................... 21
2.2 Majukumu ya Kamati ya Mkoa .................................... 21

3.0 Muundo katika Wilaya na Majukumu .................................... 22
3.1 Kamati ya Menejimenti ya Maafa ya Wilaya .................................... 22
3.2 Majukumu ya Kamati ya Wilaya .................................... 22

4.0 Ngazi ya Jamii .................................... 23
4.1 Muundo Ngazi ya Kata, Vijiji/Mitaa na Majukumu .......... 23
4.2 Kamati ya Menejimenti ya Maafa za Kata na Kijiji ........... 23
4.3 Majukumu ya Kamati za Kata na Vijiji/Mitaa .................... 24

5.0 Ngazi ya Kaya .................................... 24
5.1 Majukumu ya Kaya .................................... 24
5.2 Wajibu na Majukumu ya Kaya .................................... 24

6.0 Kongamano la Menejimenti ya Maafa .................................... 25
7.0 Tahadhari ya Awali .................................... 25
8.0 Jukumu la Mashirika yasiyo ya Kiserikali na Wadau wengine ... 25
8.1 Mashirika yasiyo ya Kiserikali .................................... 26
8.2 Vyombo vya Habari .................................... 26
8.3 Taasisi za Umoja wa Mataifa na za Kimataifa .................... 26
8.4 Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania .................................... 26

# DIBAJI

Inafahamika kuwa maafa mbalimbali yamekuwa yakiongezeka ulimwenguni kote, Tanzania ikiwemo. Nchi hii imekuwa na uzoefu wa ongezeko la maafa mbalimbali kutokana na majanga ya asili na yale yanayosababishwa na vitendo vya binadamu ambayo yamesababisha upotevu wa maisha, mali pamoja na uharibifu wa Mazingira.

Aidha, kumekuwa na udhaifu mkubwa katika kukabiliana na maafa katika ngazi zote za mzingo wa manejimenti ya maafa. Hii ni kuanzia kupunguza athari za maafa yatokeapo, kuzuia, kujiandaa, kukabiliana na maafa, kurudisha hali baada ya maafa kutokea. Udhaifu huu unatokana na muundo wa kiasasi na kisheria usiotosheleza, na utaalam mdogo wa vyombo vilivyopo, hivyo kuwepo kwa umuhimu wa hatua za haraka za kupunguza athari za maafa kwa wananchi wote.

Kuwepo kwa Sera mahususi ya maafa ni muhimu kwa ufuatiliaji na manejimenti ya maafa, lengo likiwa ni kupunguza kiwango cha athari za maafa, hivyo kupunguza umasikini. Msisitizo wa Sera ya Maafa ni kuwa na maisha salama yasiyokwazwa mara kwa mara na majanga. Hili linawezekana kwa kujenga uwezo wa asasi za umma na binafsi pamoja na jamii kwa ujumla ili kuziwezesha kutekeleza kwa ufanisi shughuli zinazohusiana na hatua zote katika Mzingo wa Menejimenti ya maafa.

Sera hii imeandaliwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kuanzia ngazi ya Wilaya, Mkoa hadi Taifa kati ya mwaka 2000 na 2003. Mchango wa kina toka kwa wadau wote umewezesha kukamilika kwa Sera hii.

Mafanikio ya Sera hii yanategemea kwa kiasi kikubwa ushirikiano na uwajibikaji wa kila mdau. Hivyo, basi, nachukua fursa hii kuwataka wadau wote kutimiza wajibu wao kwa kuifanyia kazi Sera hii.

Frederick T. Sumaye
**WAZIRI MKUU WA**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI:

Tanzania imekuwa na historia ya maafa tangu mwaka 1872. Maafa hayo yamesababisha vifo, uharibifu wa mali na mazingira. Maafa ni mlolongo wa matukio yanayoathiri jamii na kusababisha vifo, upotevu wa mali na uharibifu wa mazingira ambayo yanazidi uwezo wa jamii husika kukabiliana nayo kwa kutumia raslimali zake yenyewe. Matukio ya maafa yanaweza kuwa ya ghafla au pole pole kutegemea kasi, chanzo na madhara yake. Maafa ya asili na yale yanayosababishwa na binadamu yanaweza kutokea ghafla au polepole.

Aina ya majanga nchini Tanzania ambayo yanaweza kuleta madhara ni magonjwa ya mlipuko kwa binadamu na mifugo, ukame, moto, ajali za vyombo vya usafiri na za viwandani, mafuriko, wadudu/ndege na wanyama waharibifu wa mimea. Mengine ni ya wakimbizi, vimbunga na upepo mkali, migogoro ya jamii; tetemeko la ardhi, milipuko na volkano. Upepo mkali na tetemeko la ardhi hutokea kwa nadra sana hapa nchini, lakini aina nyingine za majanga yaliyoainishwa juu hutokea mara kwa mara.

Wakati mwingine maafa yanaweza kuwa makubwa na yenye madhara makubwa. Makali ya madhara ya maafa katika jamii yanategemea jinsi gani ilivyojiandaa kukabiliana nayo.

Kutokana na kuongezeka kwa matukio na madhara ya maafa nchini, Serikali ilipitisha Sheria Namba 9 ya mwaka 1990 ya Uratibu wa Utoaji Misaada ya Maafa. Katika Sheria hiyo, Kamati ya Maafa ya Taifa (Tanzania Disaster Relief Committee - TANDREC) ilianzishwa ili kuratibu misaada yote ya Maafa Nchini. Kamati za maafa kama hii zilitakiwa kuanzishwa katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Sera hii ya Maafa inazingatia masuala muhimu katika mzingo (cycle) wa menejimenti ya maafa yaani kuzuia, kupunguza athari, kujiandaa, kukabiliana nayo yanapotokea na urudishaji wa hali ilivyokuwa kabla ya maafa kutokea au kuiboresha zaidi.

## 1.1 Umuhimu:

Sera ya Maafa inaweka umuhimu mkubwa katika usalama wa maisha ya watu na mali zao kwa kuhakikisha kupunguza kwa

kiasi kikubwa athari za kiuchumi na kijamii. Nia ni kujenga uwezo wa uratibu na mashirikiano baina ya wadau muhimu wa maafa katika ngazi mbali mbali. Hili linawezekana kwa kuweka masuala ya

maafa katika mipango ya maendeleo ya sekta zote nchini. Kwa kuwa upunguzaji wa athari za maafa ni sawa na suala la upunguzaji umaskini, hatua za kuzuia na kupunguza athari za maafa suala ya maendeleo ambayo hayawezi kupatikana bila ya kuwa na Sera. Hivyo, ni muhimu kujikinga na kuzuia maafa mengine yasitokee.

### 1.2.1 Madhumuni na Upeo wa Sera:

### 1.2.2 Madhumuni:

(i) Kujenga uwezo wa hali ya juu wa kuzuia, kujiandaa na kukabiliana na maafa ya aina ye yote;

(ii) Kutoa elimu ya umma na kushirikisha jamii kuhusu kujikinga na maafa,

(iii) Kuwepo na muundo wenye ufanisi kwa ajili ya uratibu na mashirikiano,

(iv) Kuendeleza utafiti, utoaji taarifa na mafunzo;

(v) Kuweka masuala ya maafa katika mipango ya maendeleo katika sekta za ngazi zote.

### 1.2.3 Upeo:

(i) Kuendeleza shughuli za muda mrefu zinazolenga kupunguza madhara kwa watu na mali.

(ii) Kujenga uwezo wa kuzuia, kujikinga, kujiandaa na kukabiliana na maafa yanapotokea kwa kuwa na mpango mzuri wa mafunzo na utafiti.

(iii) Endesha shughuli za kukabiliana na maafa ili kuokoa maisha na mali kwa kuandaa na kuwa na vifaa,

chakula, maji, madawa na mahitaji muhimu kuokoa waathirika pamoja na kurejesha huduma muhimu za umma.

SURA YA PILI

# 2.0 MATAMSHI YA SERA YA MENEJIMENTI YA MAAFA

Menejimenti ya maafa inahusisha uratibu, udhibiti, utekelezaji na tathimini ya shughuli zote zinazounda mzingo wa utaratibu wa kudhibiti maafa. Utaratibu huu unazingatia uzuiaji, upunguzaji athari mara maafa yatokeapo, kujiandaa na jinsi ya kukabiliana nayo punde yanapotokea na kurudisha hali ilivyokuwa kabla ya maafa kutokea. Taratibu hizi mara zote huwa zinakwenda sambamba kwenye utekelezaji. Hatua za kwanza zinahusisha upunguzaji athari na kujiandaa kukabiliana na maafa ambazo ni shughuli za maendeleo zikifuatiwa na kukabiliana na maafa na hatimaye urudishaji wa hali ilivyokuwa kabla ya maafa kutokea. Hatua hii inahusisha shughuli za ukarabati na ujenzi. Mapitio baada ya maafa ni shughuli nyingine muhimu japo haipo moja kwa moja kwenye mzingo wa menejimenti ya maafa.

## 2.1 Vipengele vya Menejimenti Ya Maafa

### 2.1.1 **Kuzuia na Kupunguza Athari**

(a) **Hoja**:

Uzuiaji na upunguzaji athari zinazotokana na maafa unalenga katika kukabili matukio mabaya ya maafa yatokeapo kwenye jamii na mali zao. Uzoefu unaonyesha kwamba, mipango ya maendeleo ya kisekta haikidhi moja kwa moja shughuli za uzuiaji na upunguzaji wa madhara punde maafa yatokeapo. Shughuli zote za maafa toka

sekta moja hadi nyingine hazijaratibiwa vizuri. Mara nyingi hata pale ambapo kanuni za kuzuia maafa zipo, hazikaziwi vya kutosha hivyo kutoa mwanya kwa maafa kutokea.

(b) **Madhumuni**:

Kuoanisha masuala ya menejimenti ya maafa kwenye Sera, mipango na mikakati ya wadau wote ili kuboresha uzuiaji na upunguzaji athari mara maafa yatokeapo.

(c) **Tamko la Sera:**

(i) Wadau wote kuhakikisha kwamba shughuli za kuzuia na kupunguza athari za mafaa zinajumuishwa kwenye mipango yao ya kisekta;

(ii) Wadau wote kuhakikisha kwamba wanazingatia sheria na kanuni zinazosimamia masuala yote ya menejimenti ya maafa yanayohusiana na majengo, afya, usafiri, moto, matumizi ya ardhi, mazingira na mabaki ya viwandani.

### 2.1.2 Kujiandaa Kukabiliana na Maafa:

**(a) Hoja:**

Kujiandaa kukabiliana na maafa kunahusisha kuandaa hatua muhimu za kiutawala, kisheria na kiufundi zenye lengo la kupunguza madhara kwa wanaokabiliwa na maafa. Hizi ni pamoja na utoaji wa tahadhari ya awali, mafunzo, mfumo wa mawasiliano, mipango ya uokoaji, na utafutaji wa rasilimali. Zoezi hii linahitaji kurudusiwa mara kwa mara mifumo na mipango, urekebishaji, na kufanya majaribio. Kwa sasa mifumo iliyopo bado haijaendelezwa na mingine muhimu haipo kabisa. Pale inapokuwepo, haifanyiwi majaribio kuona ufanisi au dosari zake ili zirekebishwe.

**(b) Madhumuni:**

Kuhakikisha asasi zote zenye jukumu la menejimenti ya maafa zinajiandaa, ziratibiwa na zinakuwa na rasilimali na

nyenzo za kukabili maafa; mfano hospitali na vikosi vya zima moto.

**(c) Tamko la Sera:**

(i) Sheria ya Na. 9 ya Kuratibu Misada ya Maafa ya mwaka 1990 irekebishwe ili iendane na dhana nzima ya menejimenti ya maafa.

(ii) Sekta Ongozi kwa kushirikiana na wadau wengine wa maafa wawe na utaratibu mahususi wa kuanzisha na kuweka vifaa muhimu, mfumo wa tahadhari na mbinu mbali mbali za kukabiliana na maafa ya kila aina.

### 2.1.3 Kukabili Maafa:

**(a) Lengo:**

Kukabili maafa kunalenga katika kuokoa maisha na kuyashughulikia mahitaji ya dharura ya waathirika wa maafa. Shughuli zinazojumuisha kukabili maafa ni pamoja na atoaji wa tahadhari ya awali, tathmini ya haraka ya madhara na mahitaji ya waathiria; pamoja na mahitaji ya rasilimali. Nyingine ni utafutaji na uokoaji, kuhamisha watu, ugawaji wa misaada ya kibinadamu, na ujenzi wa makazi ya muda.

Uzoefu unaonyesha kwamba Sheria ya Kuratibu Misaada ya Maafa Na. 9 ya mwaka 1990 inatoa mwongozo wa jinsi ya kukabiliana na dharura, hususan ugawaji wa misaada na sio menejimenti nzima ya maafa. Muundo na majukumu katika ngazi za chini haukuzingatiwa ipasavyo na mahitaji mengine muhimu kwa ajili ya ufanisi katika kukabili maafa hayatoshelezi. Aidha sheria ina upungufu mwingine wa kukosekana ari katika utekelezaji wake na ushirikishwaji duni wa wadau wengine.

**(**b) **Madhumuni:**

Serikali ianzishe mfumo mzuri wa kisheria, kiutawala na kiasasi utakaoleta ufanisi katika kukabili maafa ili kupunguza athari punde maafa yanapotokea.

(c) **Tamko la Sera**:

(i) Serikali na wadau wengine kuanzisha mfumo wa kukabiliana na maafa ukiwa na muundo wa utoaji maelekezo, mafunzo ya kutosha kwa watumishi na zana zinazofaa kwa kukabiliana na aina zote za maafa.

(ii) Kufanya mapitio ya mara kwa mara, marekebisho, kuhuisha na kuufanyia majaribio mfumo mzima wa kubaini ufanisi wake.

(iii) Kuwa na mfumo wa ushirikiano wa kikanda ili kuwezesha upatikanaji wa msaada toka nchi nyingine pale inapobidi.

### 2.1.4 Kurejesha Hali:

**(a) Hoja:**

Hatua ya urejeshaji wa hali inalenga kwenye kuirudisha jamii iliyoathirika na maafa kwenye hali yake ya kawaida au iliyobora zaidi. Hatua hizi ni pamoja na kurudisha huduma za maji, makazi, umeme, mawasiliano, haduma za madawa.

Hatua ya kujenga na ukarabati ni ya muda mrefu inayolenga kurudisha huduma zote kama vile kujenga upya miundo mbinu iliyoharibika sana kuhuisha na kuboresha eneo lililoathirika. Uzoefu uliopo unaonyesha kuwepo na msisitizo katika kukabili maafa huku urudishaji hali, ukarabati na ukarafati vikiachwa bila kuguswa. Tabia hii imedumaza maendeleo yaliyopatikana kwa kipindi kirefu.

**(b) Madhumuni:**

Serikali ihakikishe kwamba rasilimali za kutosha zinapatikana na kuwe na utaratibu maalum wa kurejesha hali na ukarabati wa eneo lililokumbwa na mafa.

**(c) Tamko la Sera:**

(i) Sekta zinazohusika zitenge fedha za dharura na mpango maalum uanzishwe wa kuhakikisha mifumo iliyoharibiwa na maafa inarudishwa katika hali yake ya kawaida;

(ii) Halmashauri zihakikishe ushirikishaji wa waathirika wa maafa katika programu za kurejesha hali;

(iii) Mipango ya kijamii na ushauri nasaha haina budi kuanzishwa ili kuisaidia jamii iliyoathirika kurejea katika hali ya kawaida.

### 2.1.5 Tathmini Baada ya Maafa Kutokea:

**(a) Lengo:**

Uzoefu unaopatikana kutoka na maafa ya nyuma ni muhimu sana katika kuboresha hatua mbali mbali za kuchukua mara litokeapo janga lingine. Kinachofanyika ni kuanzisha tume za uchunguzi na kutafuta ukweli na sio kuwa na utoaji wa taarifa baada ya tukio wala kujifunza kutokana na uzoefu

**(b) Madhumuni:**

Serikali ifanye mapitio baada ya maafa kutokea pamoja na utoaji wa taarifa ili uzoefu unaopatikana utumike mara litokeapo janga lingine.

**(c) Tamko la Sera:**

Asasi Ongozi na wasimamizi wakuu wa tukio (Incident Commanders) waandae mapitio na taarifa za kina kwa kila tukio la maafa wanalosimamia.

### 2.1.6 Upatikanaji wa Fedha:

**(a) Lengo:**

Fedha za dharura kwa ajili ya misaada ya kukabiliana na maafa kwa wadau wote zinatakiwa zipatikane kwa haraka. Mikataba ya makubaliano kati ya serikali na wadau wengine iwepo ili kuidhinisha matumizi mazuri ya rasilimali wakati wa dharura. Hii itaiwezesha nchi kuwa na uwezo wa kupunguza athari za maafa mbali mbali pamoja na kujiandaa kuyakabili. Uzoefu unaonyesha kwamba yote haya yamekuwa hayafanyiki.

**(b) Madhumuni:**

Serikali na wadau wengine kutenga fedha za kutosha katika bajeti zao ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Lazima ziwepo fedha za kutosha kuzuia, kujiandaa na kupunguza athari za maafa.

**(c) Tamko la Sera:**

(i) Serikali ianzishe taratibu muafaka pamoja na rasilimali za kutosha kukabiliana na maafa pamoja na dharura nyingine;

(ii) Fedha na rasilimali nyingine zilizotengwa na wadau mbali mbali kwa ajili ya maafa, taarifa zake ziwe wazi kwa serikali ili iweze kuratibu vizuri matumizi yake na kuondoa uwezekano wa kulundika pamoja rasilimali ambazo zingeweza kutumika mahali pengine;

(iii) Serikali ianzishe mfuko wa menejimenti ya maafa ambapo wadau na wafadhili mbali mbali wataweza kuchangia.

### 2.1.7 Mambo ya Ujumla ya Kisera:

Maafa mara nyingi huathiri sekta mbali mbali na kuvuka mipaka ya nchi. Hivyo menejimenti yake inahusisha shughuli za asasi zaidi ya moja. Menejimenti ya maafa inahitaji ushirikiano wa sekta mbali mbali na taaluma mbali mbali kwa mwingiliano wa sera, miradi, mipango, na mikakati. Mafanikio ya utekelezaji wa sera hizi unahitaji kuwa na majadiliano na makubaliano kwa kuhusisha sheria zinazotumika katika sekta mbalimbali. Mambo ya ujumla yaliyozingatiwa ni pamoja na: -

#### 2.1.7.1 Makundi Maalum

**(a) Lengo:**

Maafa yanapotokea waathirika wakuu ni wanawake, watoto, walemavu na wazee. Makundi haya ambayo yako kwenye uwezekano mkubwa wa kuathirika kutokana na nafasi yao katika jamii yanahitaji uangalizi maalum wakati wa kukabili maafa na huhitaji msaada tofauti na wathirika wengine. Kwa mfano wakati wa mfarakano wa kijamii wanawake na watoto mara nyingi hufanyiwa vitendo vibaya vinavyokiuka haki za binadamu. Uzoefu unaonyesha kwamba hakuna uchambuzi wa kina unaogusa masuala haya wakati wa maafa.

**(b) Madhumuni**

Wadau wote wa menejimenti ya maafa watilie maanani uwezo na hali halisi ya makundi maalum katika kukabili maafa.

**(c ) Tamko la Sera:**

(i) Serikali na wadau wengine kwenye menejimenti ya maafa wazingatie mahitaji ya makundi maalum wanapotekeleza wajukumu yao;

(ii) Uangalizi mahsusi utolewe kwa makundi maalum kwenye ngazi zote za menejimenti ya maafa.

#### 2.1.7.2 Ushirikiano wa Kikanda:

**(a ) Lengo**

Ni dhahiri kwamba hakuna sehemu ya dunia isiyoweza kukabiliwa na maafa. Nchi moja moja zina uwezo mdogo wa kukabili maafa kwa kuwa maafa yana asili, tabia na matokeo ambayo huvuka mipaka ya kitaifa, hivyo ushirikiano wa kinchi na ki-eneo ni muhimu, Tanzania ni

mwanachama wa jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Ushirikiano wa Nchi za Kusini mwa Afrika , Umoja wa Afrika , na Umoja wa Mataifa . Kwenye vyombo hivi nyote kuna msisitizo mkubwa wa kuzitaka nchi wanachama kuweka utaratibu mzuri wa kukabiliana na maafa. Tatizo linalokabili jumuiya hizi za kikanda ni ukosefu wa rasilimali za kutosha na kipaumbele katika udhibiti wa maafa.

(b) **Madhumuni:**

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ijihusishe katika fora mbali mbali kuhusu menejimenti ya maafa kikanda kwa kuweka utaratibu utakao iwezesha ishiriki kikamilifu katika masuala ya maafa kikanda.

(c) **Tamko la Sera**:

Serikali iridhie na kutekeleza mikataba ya kimataifa juu ya upunguzaji majanga na mingine inayohusu maafa yanayotokea bila kujali mipaka ya nchi.

### 2.1.7.3. Mfumo wa Tahadhari

**(a) Lengo**:

Uwezo na ufanisi mzuri wa kukabili maafa unategemea kiwango cha maendeleo ya mfumo wa kutoa tahadhari. Kiwango cha athari ya maafa kinategemea tahadhari iliyotolewa na kiwango cha jamii kuzingatia tahadhari hiyo. Mifumo ya tahadhari lazima ieleweke vizuri, iendelezwe na kufanyiwa majaribio ya mara kwa mara ili iweze kuleta ufanisi. Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Kitengo cha Kutambua Matetemeko ya Ardhi kilicho chini ya Wizara ya Nishati na Madini, Mtandao wa Kutoa Tahadhari za Ukame na Njaa, Kitengo cha Kudhibiti Magonjwa ya Mimea na Idara ya Usalamai wa Chakula chini ya Wizara ya Kilimo na Chakula na Kitengo cha Dharura na Maafa chini ya wizara ya Afya ndivyo vyombo vyenye jukumu la kisheria la kutoka tahadhari ya awali. Ufanisi katika utendaji wa vitengo hivi unadumazwa na ukosefu wa vifaa vya kisasa, watalam na fedha. Aidha

mbinu za asili za kutabiri majanga hazijaendelezwa kuweza kutoa utabiri unaofaa. Kwa ujumla hakuna utararatibu makini wa kutoa tahadhari ya awali hapa nchini.

**(b) Madhumuni**:

Mifumo ya Tahadhari za awali iendelezwe na kuimarishwa ili kuhakikisha jamii inapata taarifa sahihi na mapema.

(c) **Tamko la Sera**:

(i) Wizara zenye vitengo vyenye jukumu la kutoa tahadhari za awali ziwekeze vya kutosha katika kuviimarisha ili viweze kutoa taarifa sahihi na kwa wakati muafaka;

(ii) Serikali ihakikishe mifumo ya tahadhari ya awali ya kiasili inapitiwa upya, kuendelezwa, na kuimarishwa ili iweze kutoa taarifa za kuaminika na tafsiri yake ili jamii ijiandae ipasavyo;

(iii) Serikali ianzishe ishara kwa kila janga na kuhakikisha wanajamii wazifahamu.

**2.1.7.4 Misaada kwa Waathirika wa Maafa**:

(a) **Lengo**:

Uzoefu unaonyesha kwamba hakuna utaratibu mahsusi wa kutoa misaada kwa waliopatwa na maafa. Mambo muhimu kama aina ya misaada inayotakiwa wakati inapohitajika, Mlengwa ni nani, na kipindi ambacho msaada unatakiwa hayajapatiwa ufumbuzi na mara nyingine kumekuwa na mtazamo wa kisiasa.

(b) **Madhumuni:**

Serikali iweke vigezo na kanuni za kutoa huduma za msaada na vijulikane kwa wadau wote.

(c) **Tamko la Sera:**

Serikali haina budi kuandaa mwongozo wa kusimamia utoaji wa misaada kwa waathirika wa maafa mbali mbali na ujulikane kwa walengwa wote na wahisani. Mwogozo ufafanue vipengele kama: kipindi msaada unapotakiwa, kiwango cha athari, aina na kiasi chake ili kuondoa uwezekano wa kulundikana kwa juhudi mbali mbali eneo moja na malalamio yasiyo ya lazima.

### 2.1.7.5 Hifadhi ya Mazingira:

(a) **Lengo**:

Maafa yanaharibu mazingira. Pia uharibifu wa mazingira unasababisha maafa. Hakuna juhudi za pamoja zilizochukuliwa na jamii ili kuzuia uharibifu wa mazingira ili hatimaye kupunguza uwezekano wa maafa kutokea. Aidha hakuna juhudi za makusudi za kuhifadhi mazingira baada ya maafa kutokea.

(b) **Madhumuni**:

(i) Serikali iweke kanuni za hifadhi ya mazingira ili kuyalinda maafa yatokeapo;

(ii) Serikali ifanye tathmini ya mazingira ili kuyalinda yasiharibiwe maafa yatokeapo;

(iii) Miradi inayoanzishwa na kutekelezwa izingatie tathmini na matokeo yake katika mazingira;

(iv) Serikali na wadau wengine hawana budi kutoa elimu ya hifadhi ya mazingira.

SURA YA TATU

# 3.0 MUUNDO WA MENEJIMENTI YA MAAFA:

## 3.1 Maelezo Ya Jumla:

Madhara ya maafa ni mengi na hudumu kwa muda mrefu. Kukabiliana nayo kunahitaji ushirikishwaji wa sekta nyingi kwani asasi moja haiwezi kukidhi mahitaji katika kukabilina na maafa. Ili kuepuka urasimu na kuingiliana katika majukumu, ni vema kuwepo kwa muundo unaojulikana wa kila taasisi na majukumu yake katika ngazi zote. Sera hii inaainisha muundo na majukumu muhimu kuanzia ngazi ya Taifa hadi jamii ili masuala yahusuyo maafa yaweze kushughulikiwa kikamilifu. Msisitizo utakuwa katika kuanzisha na kuimarisha miundo hii katika utoaji mafunzo, upatikanaji wa rasilimali na kuimarisha uratibu.

### 3.1.1. Kamati:

Kamati za menejimenti ya maafa zitaundwa kuanzia ngazi ya mkoa, wilaya ambapo kwa ujumla zitakuwa na majukumu ya kuratibu,

kuelekeza, kuidhinisha na kudhibiti shughuli zote za menejimenti ya maafa katika maeneo yao. Kamati hizi zitaitwa Kamati ya Maafa ya Mkoa) na Kamati ya Maafa ya Wilaya. (Angalia kiambatisho 1 na 2).

### 3.1.2 Kamisheni ya Menejimenti ya Maafa:

Idara ya Kuratibu Misaada ya Maafa kama ilivyofafanuliwa kwenye sheria na 9 ya mwaka 1990 chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, haina budi kurejewa na badala yake ianzishwe Kamisheni ya Menejimenti ya Maafa. Kamisheni hii itakuwa ndicho chombo kikuu cha kushughulikia masuala ya maafa kitaifa ambapo itahusika na masuala yote ya utekelezaji wa sera, kuratibu programu za maafa, operesheni na mipango ya kukabiliana na maafa kitaifa. Kamisheni hii vile vile itaratibu mahusiano ya kitaifa na kimataifa. (Angalia kiambatisho A2)

### 3.1.3 Asasi Ongozi:

Asasi Ongozi na zitakazosaidia, zitaainishwa kwa kila tukio muhimu la menejiment ya maafa. Asasi hizi hazina budi kuhuhisha sheria zilizopo pamoja na Kanuni za Utendaji Kazi zihusuyo maafa hayo katika sekta husika. Mwogozo wa Kitaifa wa Kudhibiti Maafa utaainisha na kufafanua wajibu na majukumu ya kila asasi.

### 3.1.4 Kamati za Kitaalamu:

Kamati za Kitaalamu zitaundwa kwa kila sekta na zitakuwa na wajibu wa kutoa ushauri wa kitaalamu kwa maafa yanayohusu sekta husika.

### 3.1.5 Vitengo vya Menejimenti ya Maafa:

Kila mdau katika menejimenti ya maafa, ataanzisha kitengo au atakuwepo ofisa mmoja mahsusi atakayehusika katika kuratibu na kufuatilia masuala ya maafa.

### 3.1.6 Timu za Kukabili Maafa

Kutakuwepo na timu za kukabiliana na dharura na maafa kila inapotokea katika ngazi zote.

### 3.1.7 Ngazi ya Jamii:

Katika ngazi ya jamii, yaani ngazi ya Kata na Vijiji ambako ndiko maafa yanapotokea, kamati za menejiment ya maafa zitaanzishwa na kuwa "mstari wa mbele" katika menejimenti ya maafa. Dhana kuu ya muundo huu (kuanzia ngazi ya taifa hadi jamii) ni ili kuhakikisha kuwa kuna utaratibu madhubuti wa kukabiliana na maafa kwa lengo la kuokoa maisha ya watu na mali zao.

## 3.2 Wajibu na Majukumu ya Wadau Wengine:

Serikali kwa upande wake itahakikisha kuwa inafahamu raia wake, taasisi, sekta binafsi, na taasisi zisizo za kiserikali pamoja na wahisani wenye ujuzi na taaluma muhimu kama rasilimali za kutumika endapo maafa yatatokea. Taasisi/asasi muhimu na majukumu yao yatakuwa kama ifuatavyo:

### 3.2.1 Vikosi vya Ulinzi na Usalama:

Vikosi vya majeshi ya ulinzi na usalama vina nafasi mahsusi. Hii ni kwa sababu vina vyombo vya usafiri, vina mfumo unaojulikana pamoja na utaalamu wa fani zote. Aidha vinaweza kufanya kazi kwa kujitegemea na kwa utaratibu waliojiwekea. Majeshi yanaweza kusaidia juhudi za jamii endapo hali ya hatari au maafa yanapotokea na, endapo wataombwa kufanya hivyo. Majeshi yanaweza kufanya kazi ya ziada pale jamii inaposhindwa kabla ya kuomba msaada kutoka nje ya nchi.

### 3.2.2 Ushiriki wa Sekta Binafsi

Sekta binafsi inao utaalam, vifaa pamoja na fedha za kuweza kusaidia juhudi za serikali. Vilevile wanawajibika kuhakikisha usalama wa mali zao pamoja na kuhakikisha kuwa wanachukua tahadhari pindi dharura au majanga yanapotokea. Hata hivyo sekta binafsi katika shughuli zake, huvutiwa sana na faida, hivyo changamoto hapa ni jinsi gani sekta hii inavyoweza kushirikishwa katika menejimenti ya maafa na hususan katika kukabiliana na majanga katika kuzifanya huduma za kibiashara zitolewe bure wakati janga linapotokea. Hii ni pamoja na huduma za hospitali na maji. Serikali itaweka utaratibu wa huduma zitakavyotolewa

kutokana na rasilimali zinazomilikiwa na watu binafsi, na kuweka utaratibu wa makubaliano maalum.

### 3.2.3. Idara ya Zima Moto na Uokoaji:

Idara ya zima moto na uokoaji inao ujuzi wa kukabiliana na majanga ya moto pamoja na kuratibu masuala yanayohusiana na moto. Idara itahakikisha kuwa inawatumia wadau mbalimbali katika kutoa huduma bora ya zima moto mijini na vijijini. Idara itahakikisha inahuisha sheria zilizopo ili kuiwezesha sekta binafsi kutoa mchango wake kikamilifu. Idara pia itasimamia kuwa sheria ya zimamoto inatekelezwa kwa ukamilifu na kila mdau.

### 3.2.4 Jeshi la Polisi:

Jeshi la Polisi lina majukumu maalumu katika kupunguza athari, kujiandaa na kukabiliana na maafa hususan katika kulinda usalama wa raia na mali zao, uokoaji, kuhamishaji, udhibiti wa makundi na majanga ya mioto. Majukumu mengine ni utoaji wa huduma ya kwanza ya dharura, huduma ya mawasiliano, na kuwahudumia majeruhi. Jeshi la polisi watafanya mafunzo na mazoezi ya mara kwa mara ili kupata mbinu mpya katika kukabiliana na maafa.

### 3.2.5 Asasi zisizo za Kiserikali

Asasi zisizo za kiserikali, zina uwezo na rasilimali za ziada ambazo ni muhimu katika kusaidia juhudi za serikali wakati wa dharura. Asasi hizi zina manufaa kwa kuwa zinajihusisha kwa karibu zaidi katika masuala ya kijamii. Zinajihusisha katika uhamasishaji jamii, utoaji mafunzo, kutoa misaada mbalimbali, na kusaidia miradi ya kujitegemea.

### 3.2.6 Taasisi za Kimataifa

Taasisi za Umoja wa Mataifa pamoja na asasi nyingine za kimataifa ni za muhimu sana katika menejimenti ya maafa, kwa kuwa hutoa misaada ya kifedha, vifaa na utaalamu. Mahusiano zaidi yatafanywa na kuimarishwa ili kuweza kupatiwa misaada zaidi na utaalamu unaohitajika kwa ajili ya kuimarisha menejimenti ya maafa nchini.

### 3.2.7 Vyombo vya Habari

Vyombo vya habari vina umuhimu mkubwa katika kufanikisha operesheni za maafa. Vina uwezo mkubwa wa kufanya mawasiliano na

kutoa taarifa kwa wadau mbalimbali kuhusiana na maafa. Vyombo vya habari havina budi kuwahamasisha wananchi kwa kutoa tahadhari na ukusanyaji rasilimali zinazoweza kusaidia katika kukabiliana na majanga.
Idara zote pamoja na asasi zitoazo mafunzo ya utoaji habari, hazina budi kuhuisha masuala ya maafa katika mitaala yao hususan katika utendaji wao wa kila siku. Vyombo vya habari vinaaswa kuwajibika zaidi katika kutoa taarifa za maafa kwani taarifa hizi ni nyeti na zinahitaji umakini wa hali ya juu zinapotolewa.

### 3.2.8 Ngazi ya Jamii na Familia

Jamii katika ngazi ya kijiji na hata mtu mmojo mmoja wanalo jukumu kwa kutumia uwezo walionao katika kulinda maisha yao na mali visiathirike na maafa. Hatua zitakazochukuliwa na jamii pamoja na mtu mmojammoja, zitasaidia katika kuamsha ari ya kukabiliana na maafa. Sera hii, inalenga katika kuimarisha uwezo wa kijamii wa kukabiliana na maafa mbalimbali kwa kujumuisha katika mipango, mategemeo na mahitaji yao pamoja na njia mbadala za kukabiliana na maafa pindi yatokeapo.

## 3.3 Taratibu za Kisheria

Ili sera hii iweze kutekelezwa kwa ukamilifu, inahitaji kuwepo nguvu ya kisheria, mwongozo, maelekezo, ushirikishwaji wa jamii, pamoja na fedha. Sheria ya maafa Na. 9 ya mwaka 1990 inayotumika hivi sasa, haina budi kufanyiwa marekebisho ili iweze kukidhi sera hii. Vilevile sheria nyinginezo zilizopo kwenye idara za serikali zinazohusiana na maafa hazina budi kufanyiwa marekebisha ili ziweze kwenda sambamba na marekebisho ya sheria mpya iliyorekebishwa. Sheria ya menejimenti ya maafa itaelekeza mikakati ya kupunguza uwezekano wa kukumbwa na maafa vilevile kuongeza uwezo wa kitaifa wa kukabiliana na kupunguza athari za maafa pindi yanapotokea. Sheria vilevile itaainisha taratibu za kifedha kwa kutaja vyanzo mbalimbali, utoaji motisha na ushirikishwaji wa jamii katika kuandaa mipango ya menejimenti ya maafa. Utaratibu wa kuridhia ushirikiano wa kikanda kwa njia ya mikataba na makubaliano yanayohusu masuala ya maafa itafafanuliwa vizuri katika sheria.

## 3.4 Ufuatiliaji na Tathmini:

Ufuatiliaji na kufanya tathmini kitaifa ni jukumu la Kamisheni ya Menejimenti ya Maafa (KMM) ambayo itatekeleza majukumu yake kwa

ushirikiano wa karibu sana na wizara zinazohusika. Katika ngazi ya mikoa, Sekretarieti za mikoa ndizo zenye jukumu la kufuatilia na kufanya tathmini. Vilevile serikali za mitaa, miji, manispaa na jiji, zitahusika na kufuatilia na kufanya tathmini katika maeneo yao. Wadau (jumuia ya kimataifa, mashirika ya dini asasi zisizo za kiserikali na za kijamii, wafanya biashara) wana majukumu makubwa katika kutekeleza masuala mbalimbali ya menejimenti ya maafa, hivyo nao watashuirikishwa katika kufuatilia na kutathmini katika nafasi zao.

Kamisheni ya Menejimenti ya Maafa kama mratibu, itahusika katika kukusanya na kuchambua taarifa mbalimbali za utekelezaji wa programu za menejimenti ya maafa. Taarifa hizi zitasaidia katika kuainisha mapungufu yaliyopo katika malengo yaliyowekwa na utekelezaji halisi. Taarifa hii itachapishwa na hatimae kujadiliwa kwenye kongamano la wadau wote. Sambamba na sera hii, haina budi vilevele kuwepo na Sheria, Mwongo wa Taifa wa Kudhibiti Maafa, Mpango wa Kukabiliana na Maafa na Ramani inayoonyesha matukio ya maafa mabalimbali. Nyaraka zote hizi hazina budi kukamilishwa na kusambazwa kwa wadau wote katika ngazi mbalimbali.

### 3.5 Majumuisho:

Ili sera hii iweze kufanyiwa kazi ipasavyo,hapana budi kuwepo fedha za kutosha kwa ajili ya kugharamia shughuli za menejimenti hususan katika kujikinga na kujiandaa katika kukabiliana na maafa. Aidha, lazima kuwepo na muundo thabiti katika ngazi zote unaoonyesha jinsi masuala ya maafa yatakavyo shughulikiwa. Sheria hainabudi kuwepo ili sera hii iweza kutekelezeka. Mwisho patakuwepo na uhamasishaji wa jamii katika kukabiliana na maafa hasa katika maeneo ya kuzuia na kupunguza athari za maafa pindi yatokeapo, kujiandaa katika kukabiliana nayo.

Kiambatisho Na. 1

Kiambatisho Na. 2

## MAJUKUMU YA KAMATI NA WADAU WENGINE

### 1.0 Tume ya Menejimenti ya Maafa

### 1.1 **Jukumu la Jumla**:

Jukumu la jumla la Tume ya Menejimenti ya Maafa litakuwa ni uratibu na utekelezaji wa programu za udhibiti wa maafa zinazohusisha sekta nyingi. Hii ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa Sera na mikakati katika ngazi mbali mbali.

### 1.2 **Majukumu Mahususi**:

Majukumu maalumu ya Tume yatakuwa kama ifuatavyo:

(i) Kuratibu masuala yote ya udhibiti wa maafa nchini;

(ii) Kuwezesha ujengaji wa uwezo katika ngazi zote, ambazo ni Taifa, Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji;

(iii) Kuwianisha mipango ya maendeleo ya sekta katika ngazi mbali mbali za utawala;

(iv) Kuhakikisha mifumo ya udhibiti wa habari inajumuishwa katika programu za kijamii za kuelimisha Umma;

(v) Kuainisha na kuweka alama na ramani majanga yote yalipo nchini na kufanya uchambuzi wa urahisi/uwezekano wa kuwepo na hatari mara kwa mara na kwa wakati uliopangwa;

(vi) Kuhakikisha kamati za maafa katika ngazi za Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji zinaundwa kwa hatua;

(vii) Kuhakikisha taratibu zinaandaliwa zinazofaa kwa ajili ya kuendeleza timu za kujitolea za udhibiti wa Maafa;

(viii) Kuwa Mtunzaji Mkuu wa kumbukumbu na habari zinazopatikana wakati huo na inapowezekana kutawanya kwa wakati habari hizo kwa wadau kupitia, magazeti, vipeperushi, mikutano, na vyombo vingine vya uenezaji wa habari kama inavyofaa.

(ix) Kufanya kazi nyingine yoyote itakayotakiwa kuifanya.

## 2.0 **Muundo Katika Mikoa na Majukumu**:

### 2.1 Kamati ya Menejimenti ya Maafa ya Mkoa

Sekretariati ya Mkoa, wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Mamlaka za Mitaa, wataunda Kamati ya Maafa ya Mkoa chini ya uenyekiti wa Mkuu wa Mkoa. Wajumbe watakao karibishwa kwenye kamati na mwenyekiti watakuwa ni Asasi za Kijamii (Mashirika yasiyo ya Kiserikali na Vikundi vya Kijamii), wawakilishi wa jumuiya za wafanyabiashara, viongozi wa mashirika ya dini na watu maarufu katika mikoa.

Kamati ya Maafa ya Mkoa itakuwa ndiyo chombo cha utekelezaji na usimamizi wa mali za Udhibiti wa Maafa katika mkoa. Kila kamati ya mkoa itakuwa ni njia ya habari na raslimali na kiungo katika utekelezaji wa madhumuni na malengo na vipaumbele kati ya wilaya na Taifa. Ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu Mamlaka ya mkoa itateua mtu mmoja hususan Afisa Mipango au itaanzisha kitengo kitakachohusika na uratibu wa udhibiti wa shughuli za maafa katika mkoa.

### 2.2 **Majukumu ya Kamati ya Maafa ya Mkoa**:

Kama Asasi Ongozi katika mkoa, Kamati ya Maafa ya Mkoa itakuwa na majukumu yafuatayo:-

(i) Kufuatilia kwa wakati wote majanga, hatari na matishio ya maafa na hali za uwezekano wa watu kukumbwa na maafa katika mkoa;

(ii) Kufanya uchambuzi kutokea kwa maafa katika maeneo sugu na kutoa maoni na mapendekezo juu ya kupunguza uwezekano wa watu kupatwa na maafa;

(iii) Kuainisha mahitaji ya mafunzo na kuendesha/kutoa elimu, mafunzo na kuelemisha Umma;

(iv) Kukusanya zana na kuratibu hatua mbali mbali zinazofanywa na Asasi nyingine;

(v) Kuhakikisha udhibiti wa maafa unakuwa ni imara, na kuonekana katika vipaumbele na miongozo ya mkoa na Taifa;

(vi) Kuunga mkono utekelezaji wa programu za udhibiti wa maafa zilizokubaliwa katika mkoa.

(vii) Kukusanya raslimali za kifedha na vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya udhibiti wa maafa.

3.0 **Muundo Katika Wilaya na Majukumu**:

**3.1 Kamati ya Menejimenti ya Maafa ya Wilaya**

Halmashauri za wilaya zina jukumu la uainishaji, ukutekelezaji, ufutiliaji na upimaji wa programu za maendeleo za wilaya. Hivyo, timu ya menejimenti ya wilaya itakuwa ni kamati ya menejimenti ya maafa ya wilaya chini ya uenyekiti wa mkuu wa wilaya na mkurugenzi mtendaji wa wilaya atakuwa ni katibu. Wajumbe zaidi watatoka katika mashiriki ya kijamii, wawakilishi wa jumuiya ya wafanyabiashara, viongozi wa mashirika ya dini na watu maarufu katika wilaya.

3.2 **Majukumu ya Kamati ya Maafa ya Wilaya**

Kamati ya udhibiti wa Maafa ya Wilaya itakuwa na majukumu yafuatayo:

(i) Kuhuisha masuala ya Udhibiti wa Maafa katika mipango ya wilaya;

(ii) Kufuatilia kwa wakati wote, majanga, hatari, na matishio ya maafa na hali za uwezekano wa watu kukumbwa na maafa katika wilaya;

(iii) Kufanya uchunguzi juu ya kutokea kwa maafa katika maeneo sugu na kutayarisha maoni na mapendekeza ya jinsi ya kupunguza urahisi/uwezekano wa watu kukumbwa na maafa;

(iv) Kuainisha na kuchora ramani ya maeneo yenye majanga katika wilaya na kufanya uchambuzi wa hatari na uwezekano wa maafa kutokea kwa watu;

(v) Kuainisha mahitaji ya mafunzo na kutoa elimu, mafunzo na programu za kuelimisha jamii;

(vi) Kukusanya mali zinazohitajika za kifedha na vifaa kwa ajili ya kudhibiti maafa;

(vii) Wakati maafa/dharura yakitokea Kamati ya Maafa ya Wilaya katika wilaya iliyoathirika, watakuwa na jukumu la kuthibitisha operesheni na hali iliyojitokeza kuhakikisha msaada unapatikana mara moja kwa jamii zilizoathirika;

(viii) Kuunda timu ya ukabilianaji wa maafa na muundo wa kulinda jamii.(civil protection system).

## 4.0 **Ngazi ya Jamii**:

### 4.1 **Muundo Ngazi ya Kata, Vijiji/Mitaa na Majukumu**:

Asasi katika ngazi hii ndizo zilizo mstari wa mbele katika kudhibiti maafa, hapa ndipo kwa kweli shughuli za maafa zinapotakiwa kutekelezwa. Kamati za udhibiti wa maafa lazima ziundwe katika ngazi za kata na vijiji/mitaa. Wilaya zitahakikisha uundaji wa miundo inayofaa

katika kuzuia, kupunguza, utayari na ukabilianaji wa Maafa. Vile vile miundo ya kulinda jamii katika ngazi hizi.

4.2 **Kamati ya Menejimenti ya Maafa za Kata na Kijiji**

Katika ngazi ya kata mwenyekiti wa kamati atakuwa ni diwani na katibu atakuwa ni mtendaji wa kata. Wajumbe watakuwa ni wenyeviti na makatibu wa vijiji pamoja na wataalam waliopo katika ngazi hiyo. Mwenyekiti wa kijiji/mtaa atakuwa mwenyekiti wa kamati katika ngazi hii. Wenyeviti wa vitongoji watakuwa wajumbe. Afisa mtendaji wa kijiji atakuwa katibu wa kamati. Wajumbe wengine watajumuisha, mashirika yasiyo ya kiserikali na ya kijamii, viongozi wa dini na wa kijadi.

4.3 **Majukumu ya Kamati za Maafa za Kata na Vijiji/Mitaa**:

Kamati katika ngazi hizi itakuwa na majukumu yafuatayo:-

(i) Kuandaa mipango na taratibu kwa ajili ya programu na maafa katika maeneo yao;

(ii) Kukabiliana na maafa au dharura inapotokea ili kuhakikisha msaada unatolewa kwenye kaya zilizoathirika;

(iii) Kuainisha na kuweka ramani za majanga yote katika maeneo yao na kufanya uchambuzi wa hatari na urahisi/uwezekano wa kutokea maafa kwenye jamii;

(iv) Kuunda vikundi vya kijamii kwa ajili ya kupunguza matokeo ya maafa na operesheni.

5.0 **Majukumu ya Kaya**:

5.1 Kaya zina majukumu ya kuchukua hatua, kulingana na uwezo wao, kulinda maisha yao na mali zao. Ni walengwa kwa ajili ya elimu ya msingi juu ya maafa, mafunzo rasmi na yasiyo rasmi, elimu kwa umma, programu za uhamasishaji lazima zilenge katika kila kaya. Dhana ya upunguzaji, uzuiaji na ukabilianaji wa awali vinahitajika katika jamii katika ngazi hii.

5.2 **Wajibu wa majukumu ya kaya**:

(i) Kupambana na matokeo ya mwanzo ya maafa hadi hapo msaada unapokuja toka ngazi nyingine;

(ii) Kutoa taarifa/habari kuhusu majanga yanayowakabili katika maeneo kwa uongozi wa juu ili taarifa hizo ziweze kuingizwa katika programu za ngazi za juu;

(iii) Kubadilishana uzoefu na ujuzi juu ya jinsi wanavyoweza kukabiliana na janga ili kutia nguvu katika uzoefu uliopo kwa ajili ya kulinda kaya dhidi ya maafa yanayowakabili kwa ufanisi;

(iv) Kushiriki katika mazoezi ya vitendo yaliyoandaliwa, kuelimisha na kutoa mafunzo kama njia ya kujenga uwezo wao.

## 6.0 **Kongamano la Udhibiti wa Maafa**:

Kongamano la udhibiti wa maafa litaundwa kwa lengo la ya kushirikiana katika kupeana habari na kubadilishana uzoefu. Kongamano litakuwa ni chanzo cha habari kwa Tume, jamii na wadau wengine. Tume itakuwa na jukumu la kuitisha kongamano angalau mara moja kwa mwaka. Washiriki watakaribishwa kutoka wadau wote pamoja na sekta binafsi.

## **7.0 Tahadhari ya Awali:**

Tahadhari ya awali ni jukumu la mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), Wizara ya Kilimo na chakula, na Wizara ya Afya. Mamlaka ya Hali ya Hewa inatakiwa kutoa tahadhari ya awali na ufuatiliaji dhidi ya majanga yatokanayo na hali ya hewa. Kazi zake ni kutabiri hali ya hewa kufutilia, kuchambua, kutafisiri na kutoa takwimu zote zinazohusiana na hali ya hewa. Wizara ya Kilimo na Chakula, kutabiri mwelekeo wa baadaye na upungufu wa chakula unaoweza kujitokeza katika maeneo maalumu. Jukumu la Wizara ya Afya ni kutoa tahadhari ya awali juu ya milipuko ya magonjwa.

## 8.0 **Jukumu la Mashirika yasiyo ya Kiserikali na Wadau Wengine**:

### 8.1 **Mashirika yasiyo ya Kiserikali**

Mashirika haya ni mshiriki muhimu katika shughuli za udhibiti wa maafa. Mashirika haya yana uwezo wa kuitikia na kukabiliana haraka na

maafa wakati yanapotokea. Ili kuimarisha uhusiano wa karibu kati yake na mamlaka za udhibiti wa maafa, itabidi kuwepo na utaratibu maalumu wa jinsi ya kushirikiana. Muungano wa mashirika yasiyo ya kiserikali ambao unawakilisha mashirika yote utafanya yafuatavyo:

(i) Kusaidia/kutia moyo wanachama wake ili washiriki katika shughuli za udhibiti wa maafa kwa lengo la kupunguza uwezekano wa kupatwa na maafa katika jamii na kwa watu binafsi. Kwa hadidu rasmi mashirika yasiyo ya kiserikali yanategemewa kushiriki katika shughuli za kutoa mafunzo kuelimisha Umma, kutathimini uharibifu, kukarabati na kukarafati katika maeneo yaliyokubwa na maafa;

(ii) Ni vema ikaeleweka kuwa mashirika yasiyo ya kiserikali na wadau wengine watafuata viwango vya kimataifa katika kutoa misaada na kuzingatia haki za binadamu.

8.2 **Vyombo vya Habari**:

Magazeti, radio na televisheni vina jukumu muhimu la kufanya katika shughuli za udhibiti wa Maafa kitaifa. Maeneo yao muhimu ya kuzingatia yatajumuisha:

(i) Uwekaji wa kumbukumbu, utoaji taarifa, uhamasishaji na utangazaji wa matukio katika shughuli za udhibiti wa maafa yote kwa ujumla na kusaidia katika programu za uelimishaji wa Umma;

(ii) Kuhuisha masuala ya maafa katika mipango na bajeti zao;

(iii) Kushiriki katika kongamano la udhibiti wa maafa ili kuhakikisha ufanisi wa mchango wa vyombo vya habari.

8.3 **Taasisi za Umoja wa Mataifa na za Kimataifa**:

Taasisi za Umoja wa Mataifa na zile za kimataifa ni muhimu katika udhibiti wa programu za maafa. Taasisi hizi zitafanya majukumu yafuatayo:-

(i) Kushiriki katika Kongamano la taifa la udhibiti wa maafa kwa ajili ya kutoa habari na kushirikiana katika uzoefu juu ya maafa;

(ii) Kushiriki katika kamati za wataalamu ambazo zinahusika na maafa maalumu;

(iii) Kutoa misaada ya kifedha na utaalamu kwa ajili ya udhibiti wa maafa nchini.

8.4 **Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania**:

Sheria liyoanzisha Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania imekipa mamlaka ya kuwajibika katika masuala ya kibinadamu katika maafa na dharura kwa kutoa huduma ya kujitolea kwa umma. Chama kina mtandao wa kitaifa na kimataifa ambao ni chanzo kizuri cha kupata nguvu kazi yenye ujuzi na fedha na rasilimali nyingine.
Chama hiki kitajihusisha na mstali wa mbele katika kuhamasisha na kuiandaa jamii katika masuala muhimu ya uzuiaji, upunguzaji, utayari na ukabilianaji wa maafa. Pia kitajihusisha katika kutoa huduma katika maeneo mengine ambayo chama kina ujuzi nayo.

# Magonjwa ya Mlipuko

